# MATATIZO YA UAINISHAJI WA VIELEZI KATIKA KISWAHILI

*Y. P. Msanjila*
*Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam*

## 1.0 Utangulizi

Madhumuni ya makala hii ni kuchangia mambo makuu mawili. Kwanza, nataka nionyeshe matatizo ya msingi yanayojitokeza katika uainishaji wa vielezi kwa ujumla. Kama ambavyo uainishaji wa maneno mengine ulivyo na matatizo, pia uainishaji wa vielezi una kasoro za hapa na pale. Lakini, mimi nafikiri tatizo kubwa linatokana na dhana yenyewe ya vielezi kwamba haiko wazi. Tunatumia vigezo gani tunapoyaita maneno haya kuwa ni vielezi na mengine siyo vielezi. Je, vigezo hivyo ni thabiti? Kama siyo thabiti, je, hakuna njia nyingine ya kupata vigezo vilivyo thabiti zaidi ambavyo vinaweza kutumika ili kuondoa matatizo yanayojitokeza? Kwa kifupi, haya ni baadhi tu ya maswali ya msingi ambayo yamejadiliwa kwa undani katika makala hii. Kusudi la pili la makala hii ni kutoa mapendekezo yangu yanayohusu namna nyingine ya kuviainisha vielezi vya Kiswahili.

## 2.0 Dhana ya maneno

Vielezi ni aina mojawapo ya aina saba za maneno katika lugha. Kuelewa dhana ya vielezi, msomaji hana budi kwanza kuelewa dhana ya maneno kwa ujumla na jinsi yanavyohusiana na kuathiriana kitungo na kimatumizi. Aina hizi saba za maneno huunda seti za maneno ambayo kila seti hufanya kazi tofauti. Kimatumizi, seti hizi za maneno huingiliana kutoka seti moja hadi seti nyingine. Ni kawaida katika tungo mbalimbali kukuta maneno yanayoitwa Nomino (N) kuitwa Vitenzi (T) na vitenzi kuitwa nomino. Chunguza mifano ifuatayo:

N
1. *Kuimba* kwenu kunanipendeza

T
2. Juma anataka *kuimba*

Katika mifano ya hapo juu, sentensi ya (1) hapo juu, neno *kuimba* limetumika kuashiria nomino ya maarifa na linavumishwa na kivumishi *kwenu*. Katika sentensi yetu ya (2), neno *kuimba* kama lilivyotumika ni kitenzi. Tunadai kuwa ni kitenzi kwa

sababu ya muundo wa sentensi yenyewe. Kimuundo, kitenzi *kuimba* kimetanguliwa na kitenzi kishirikishi *anataka*. Kuingiliana huku kwa maneno hakujitokezi tu katika seti za nomino na vitenzi peke yake bali pia katika seti nyingine za maneno. Tuchunguze tena mifano ifuatayo:

3. *Hapa* wapi?
4 Mtoto amelala *hapa*
5. *Shuleni* mbali
6. Mwalimu amekwenda *shuleni*

Kwa kuzingatia matumizi, sentensi yetu ya (3) hapo juu, neno *hapa* ni kiwakilishi-onyeshi cha mahali. Lakini neno hilohilo *hapa* katika sentensi ya (4) limetumika kama kielezi cha mahali. Tukija katika sentensi yetu ya (5) neno *shuleni* limetumika kama nomino ya mahali. Kwa upande mwingine, neno hilohilo *shuleni* katika sentensi ya (6) limetumika kufanya kazi ya uelezi na kwa mujibu wa matumizi, tumeliainisha kuwa ni kielezi cha mahali. Mifano katika (1-6) inatuthibitishia kitu kimoja cha msingi kwamba maneno yanapokuwa katika tungo huathiriana kimaana na kikazi (dhima). Na hii huwezekana pale tu maneno yanapobadilishana nafasi zao.

**3.0 Dhana ya vielezi**

Mjadala wetu hapo juu sasa unatuleta kwenye kiini cha makala yenyewe. Hebu kwanza tujiulize swali la msingi, vielezi ni nini? Wataalamu mbalimbali wakiwemo Ashton, (1947); Nkwera, (1978); Myachina, (1981); Kapinga; (1983) na Kihore na wenzie (2001) wanajibu kwamba vielezi *ni aina mojawapo ya maneno yanayoelezea zaidi juu ya vitenzi; vivumishi na vielezi vingine*. Kama fasili ya vielezi inavyoonyesha hapo juu ni dhahiri kwamba dhana ya vielezi ni pana mno kiasi kwamba inavuka mipaka ya kufafanua vitenzi peke yake. Akizungumzia lugha ya Kiingereza, Lyons (1972:326) anasema:

> Maneno yanayounda kundi la vielezi ni ya mchanganyiko; na hatudhani kama kuna nadharia ya jumla ya sarufi miundo inayoweza kuyaweka maneno hayo pamoja kama kundi moja lenye muundo unaofanana kwa maumbo yote ambayo kimapokeo yaliainishwa kama vielezi.

Madai haya ya Lyons (1972) yanaungwa mkono na wataalamu wa sarufi ya Kiswahili pale wanapoeleza kuwa mbali na vielezi kufafanua zaidi juu ya vitenzi, pia vielezi hufafanua *vivumishi* na *vielezi vingine* kama mifano ya (7) na (8) inavyoonyesha.

T N V E
7. Amejenga nyumba kubwa *mno*

N T E E
8. Musa anacheza *vizuri* *sana*

Katika mifano ya hapo juu (7 na 8), vielezi vimefafanuliwa kwa kuzingatia maana. Kielezi *mno* katika sentensi ya (7) kimetumika kufafanua kwa msisitizo juu ya kivumishi *kubwa*. Siyo tu nyumba kubwa bali ni kubwa mno (kupita ukubwa wa kawaida). Hali kadhalika, sentensi ya (8), kielezi *vizuri* kinafafanua juu ya kitenzi *cheza* na kielezi *sana* kinafafanua kwa msisitizo juu ya kielezi *vizuri*. Siyo tu anacheza vizuri bali vizuri sana (kupita uchezaji wa kawaida). Mifano ya (7) na (8) ni baadhi tu ya mifano mingi inayotumiwa na wazungumzaji wa lugha. Huu ni ushahidi kamili wa kuonyesha kuwa vielezi vinaweza pia kutumika kufafanua zaidi juu ya *vivumishi* na *vielezi vingine*

Tumesema hapo juu kwamba dhana ya vielezi ni pana na kwamba kundi linalounda vielezi ni la mchanganyiko wa maneno. Hii ni kweli kabisa. Uchunguzi wetu unaonyesha kuwa vielezi haviishii tu katika kuelezea zaidi juu ya *vitenzi*, *vivumishi* na *vielezi vingine* peke yake bali pia kwa kiasi fulani vielezi vinatumika kufafanua zaidi juu ya *nomino* na *viwakilishi* (W). Chunguza mifano ifuatayo ya (9), (10) na (11).

T E N
9. Anampenda *hasa* Matonya

T E E N
10. Anapika *vizuri* *kuliko* Mariamu

E W T E
11. *Yamkini* yeye hakucheza *vibaya*

Inafaa tukumbushie hapa kwamba mifano iliyotolewa hapo juu (9-11) imefafanuliwa kwa kuzingatia msingi wa maana. Kwa mfano, kielezi *hasa* kilivyotumika katika mfano wetu wa (9), kimetumika kutoa msisitizo kwa *nomino* Matonya na siyo kwa *kitenzi* penda. Hatuwezi kusema kwamba kwa kuwa neno *hasa* linatoa msisitizo kwa nomino basi *hasa* ni kivumishi, la hasha. Siku zote vivumishi vya Kiswahili hufuata muundo wa N+V (kwa mfano tunasema: Mtoto *mzuri*) na siyo V+N (*mzuri* Mtoto). Tunachosema hapa ni kwamba *hasa* katika mfano wa (9) ni kielezi kinachotoa msisitizo wa uvumishi kwa nomino Matonya.

Hali kadhalika, kielezi *kuliko* katika sentensi ya (10) kinatoa msisitizo wa uvumishi kwa *nomino* Mariamu zaidi kuliko kutoa ufafanuzi kwa *kitenzi* pika au

*kivumishi* vizuri. Vile vile katika sentensi ya (11), kielezi *yamkini* pia hutoa msisitizo wa uvumishi kwa *kiwakilishi* yeye. Kwa ujumla, mifano ya (9), (10) na (11) inatuonyesha dhahiri kuwa katika Kiswahili tuna baadhi ya vielezi ambavyo hufanya kazi ya uvumishi lakini vyenyewe siyo vivumishi. Hali hii ya vielezi ya kuingiliana katika dhima na maneno ya aina nyingine ndiyo iliyomfanya Lyons (1972) aseme siyo kazi rahisi kuviainisha vielezi katika kundi moja lenye muundo unaofanana kwa maumbo yote.

## 4.0 Matatizo ya uainishaji wa vielezi

Mpaka sasa tumekwishaona kwamba dhana ya vielezi ni pana na ni dhana ambayo haiko wazi. Kwa mujibu wa matumizi na kama tulivyojadili katika mifano yetu ya (7 hadi 11), dhima ya vielezi ni kutoa ufafanuzi zaidi juu ya vitenzi na aina nyingine za maneno. Kwa maoni yangu, huu uwezekano wa vielezi kutumika kufafanua aina nyingi za maneno, ndio msingi mkuu unaozua matatizo katika uainishaji wa vielezi kama tutakavyoona katika vifungu vinavyofuata.

### *4.1 Hakuna msingi mmoja wa uainishaji ulio imara*

Pengine mtu atauliza swali je, tunatumia kigezo gani tunapoainisha vielezi? Hapana shaka wataalamu wengi wa lugha (wakiwemo Ashton 1947; Myachina 1981; Kapinga 1983; na Kihore na wenzie 2001) wanatumia kigezo cha maana siyo tu wanapoainisha vielezi bali pia wanapoainisha aina nyingine za maneno. Jambo la msingi la kukumbuka hapa ni kwamba matatizo ya uainishaji wa vielezi kama tulivyogusia huko nyuma yanatokana na dhana yenyewe ya vielezi ambayo haiko wazi. Kwa mfano, Kapinga (1983) ameainisha vielezi katika aina kuu nne zifuatazo: vielezi namna, vielezi kiasi, vielezi mahali na vielezi wakati. Kapinga amezingatia msingi wa maana katika kitenzi jinsi kinavyotendeka: tendo linafanyika namna gani, wapi, mara ngapi na lini. Kasoro ya mtazamo huu ni kwamba uainisho huu unahusisha hata maneno mengine yanayofafanua juu ya maneno ya aina nyingine nayo yaitwe vielezi wakati maneno hayo hayafafanui maana ya kitenzi moja kwa moja. Tukitumia mifano yetu ya nyuma ya (7 na 8) tunagundua kuwa vielezi *mno* na *sana* havifanyi kazi ya kufafanua maana ya kitenzi moja kwa moja bali vinafafanua zaidi juu ya *kivumishi* (kubwa) na *kielezi* (vizuri). Huu ndio upungufu wa uainisho wa kimapokeo wa vielezi unaoingiza baadhi ya maneno katika orodha ya vielezi ambayo kusema kweli maneno hayo hayaelezei zaidi juu ya vitenzi moja kwa moja.

### *4.2 Dhana ya vielezi ni pana*

Maneno ambayo ni nomino, Vitenzi na Viwakilishi yanatambuliwa kuwa ni aina fulani ya maneno hata kama maneno hayo yakikaa nje ya tungo. Sifa hii ya utambuzi haiwezi kutumika kwa vielezi vyote. Kwa mfano, *vielezi mahali* visipotumika katika sentensi,

huainishwa katika aina nyingine za maneno. Chunguza mifano ifuatayo:

12. *kule* (kiwakilishi - onyeshi cha mahali)

13. *shuleni* (nomino ya mahali)

E
14. Baba amelala *kule*

E
15. Mwalimu amekwenda *shuleni*

Maneno *kule* na *shuleni* katika sentensi za (12) na (13), sasa yamechukua *dhima ya uelezi* katika sentensi za (14) na (15) tofauti na ile dhima ya mwanzo.

Ingawa vielezi vingi hutambuliwa vikiwa katika tungo, yapo maneno machache kama vile: *mno, sawa, sana, kabisa* n.k. ambayo hutambuliwa moja kwa moja kuwa ni vielezi hata kama yakikaa nje ya tungo. Mifano hii inatudhihirishia kwamba vielezi *mno, sawa, sana, kabisa* n.k. viko katika darajia tofauti na vielezi mahali (*hapa, kule, shuleni* n.k.) Kama vielezi havitambuliwi kwa sifa bainifu za aina moja, basi ni dhahiri kwamba hata maneno yanayounda seti ya vielezi yatatofautiana kimaumbo. Mjadala huu unakusudia kuonyesha namna nyingine ya kuainishia vielezi kama inavyojadiliwa katika kifungu cha 5 kinachofuata.

## 5.0 Mapendekezo ya uainishaji wa vielezi

Kutokana na dhana ya vielezi kuwa pana na kwamba kitungo maneno yake huingiliana kikazi na aina nyingine za maneno, kuna haja ya kuchunguza upya uainishaji wa vielezi. Makala hii inapendekeza kwamba uainishaji wa vielezi uzingatie kigezo cha maana ili kuweza kuviweka pamoja vielezi vyote vitokanavyo na maumbo tofauti ya maneno. Yafaa isisitizwe hapa kwamba dhana ya vielezi ni dhana ya uelezi na msisitizo juu ya vitenzi na maneno mengine. Ni kutokana na msingi huu basi hata aina nyingine za maneno kama vile *nomino* na *viwakilishi* navyo vinaweza kufafanuliwa kwa msisitizo kama ilivyo kwa vitenzi, vivumishi na vielezi vingine ili kufikisha maana iliyokusudiwa. Kwa kuzingatia mtazamo huu mpana wa dhana ya vielezi, tunaweza kuviainisha vielezi katika aina kuu mbili: *vielezi halisi* na *vielezi tumizi*. Vifungu vinavyofuata vinajadili aina hizi za vielezi kama ifuatavyo:

### *5.1 Vielezi halisi*

Katika kuyatofautisha makundi haya mawili, *vielezi halisi* ni yale maneno ambayo hutumika kuelezea namna, kiasi au jinsi tendo linavyofanyika. Kwa maelezo zaidi ni

kwamba vielezi halisi pia hutumika kufafanua zaidi namna au jinsi *kivumishi* au *kielezi kingine* kilivyo. Tunapenda kusisitiza hapa kwamba msingi wa kuviita vielezi halisi unatokana na maneno yenyewe kwamba yana uhusiano wa moja kwa moja na ama kitenzi, kivumishi, kielezi kingine na kwa kiasi fulani yana uhusiano na nomino na kiwakilishi. Mifano ya vielezi halisi ni kama hii ifuatayo:

16.

| | |
|---|---|
| mno | zaidi |
| sana | kabisa |
| hasa | lakini |
| sawa | yamkini |
| bure | sasa |
| hima | ovyo |
| hususani | haraka n.k. |

Dhana ya vielezi inafaa itokane na haya maneno yanayounda kundi hili la vielezi halisi. Hii ni kwa sababu vielezi halisi vina sifa za msingi zinazofanana na zinazoweza kutumiwa kama vigezo muhimu vya kuainishia vielezi halisi na vile vielezi visivyo halisi. Kimsingi vielezi halisi vina sifa moja muhimu ya kuelezea zaidi juu ya vitenzi na kutoa msisitizo kwa aina nyingine za maneno kama vile kivumishi, kielezi kingine na kwa kiasi fulani hata kwa nomino na kiwakilishi kuliko ilivyo kwa *vielezi tumizi*.

### *5.2 Vielezi tumizi*

*Vielezi tumizi* ni yale maneno ambayo hayana sifa za msingi za kuwa vielezi halisi lakini yakikaa katika tungo yanafanya kazi ya uelezi. Tunaweza kuvigawa vielezi tumizi katika aina kuu nne zifuatazo: vielezi tumizi mahali, vielezi tumizi wakati, vielezi tumizi ki-/v- na vielezi tumizi igizi. Hebu sasa tuangalie aina hizi za vielezi tumizi moja baada ya nyingine.

#### *5.2.1 Vielezi tumizi mahali*

*Vielezi tumizi mahali* ni yale maneno ambayo yakikaa katika tungo hujibu swali la msingi linalotambulisha vielezi yaani, tendo limetendeka/limefanyika wapi? Maneno yote yanayo jibu swali hili la msingi ndiyo huainishwa kuwa ni *vielezi tumizi mahali*. Maneno ya aina hii yanatokana na *nomino za mahali* na baadhi ya nomino hizo huishia na-***ni*** mwishoni. Chunguza mifano ya *vielezi tumizi mahali* katika mfano wa (17) hapa chini:

17. (a) Baba analima *shambani*
(b) Mwalimu amekwenda *shuleni*
(c) Musa anaishi *Bukoba*
(d) Mjomba anafundisha *Ulaya*

Katika mfano wa (17) hapo juu, maneno *shambani, shuleni, Bukoba* na *Ulaya* ni nomino za mahali. Lakini, kwa kuzingatia matumizi katika tungo, nomino hizo za mahali

zinafanya kazi ya uelezi (ya kujibu swali la msingi: tendo limefanyika wapi?) ingawa nomino hizo za mahali zenyewe siyo vielezi halisi. Nomino hizo za mahali zinapata dhima ya uelezi pale tu zinapotumika katika tungo na ndiyo sababu inayotufanya tuziite nomino hizo *vielezi tumizi mahali*.

### *5.2.2 Vielezi tumizi wakati*

*Vielezi tumizi wakati* ni yale maneno ambayo yakikaa katika tungo hujibu swali la msingi linalounda vielezi tumizi yaani, tendo limefanyika lini/wakati gani? Kimsingi, maneno yote yanayojibu swali hili la msingi, ndiyo huainishwa kuwa ni *vielezi tumizi wakati*. Maneno ya aina hii yanatokana na nomino zinazotaja wakati, siku za juma, miezi na majira ya mwaka. Tuangalie mifano ya tungo zifuatazo:

18. (a) Amefika *mchana*
    (b) Tutacheza *kesho*
    (c) Watoto watasafiri *Jumamosi*
    (d) Mvua itanyesha *masika*

Katika (18) hapo juu, maneno *mchana, kesho, Jumamosi* na *masika* ni nomino za wakati. Ukizingatia matumizi katika tungo, nomino hizo za wakati zinafanya kazi ya uelezi kwa vitenzi vilivyotumika navyo (zinajibu swali la msingi, tendo limefanyika wakati gani/lini?) ingawa nomino zenyewe siyo vielezi halisi. Kwa ufafanuzi zaidi ni kwamba nomino hizi za wakati katika (18) hapo juu, zinapata dhima ya uelezi pale tu nomino hizo zinapotumika katika tungo.

### *5.2.3 Vielezi tumizi ki-/v-*

Hivi ni vielezi tumizi vitokanavyo na maneno yanayochukua viambishi awali vya ***ki-*** (kwa nomino) na ***v-*** (kwa vivumishi) na kufanya maneno yanayoundwa yafafanue zaidi juu ya vitenzi vilivyotumika navyo katika tungo. Tungependa tusisitize hapa kwamba siyo nomino zote wala siyo vivumishi vyote vinaweza kuchukua viambishi awali vya ***ki-/v-*** ili kuunda kundi hili la vielezi tumizi. Maneno yanayokubalika ni yale ambayo yakikaa katika tungo husaidia kufafanua au kutoa uelezi wa moja kwa moja kwa vitenzi vinavyohusika navyo. Kwa ufafanuzi zaidi juu ya aina hii ya vielezi, tuangalie mifano ifuatayo:

19. (a) Anacheza *kitoto*
    (b) Wachezaji wameshindwa *kishujaa*
    (c) Mwalimu amefundisha *vizuri*
    (d) Amefanya *vema*
    (e) Amecheza *vibaya* leo

Kama mifano ya (19) inavyoonyesha, vielezi tumizi *kitoto*(-toto), *kishujaa* (-shujaa), *vizuri* (-zuri), *vema* (-ema) na *vibaya* (-baya) vimeundwa kutokana na viambishi awali ***ki-*** na ***v-***. Kielezi tumizi *kitoto* kinajibu swali la msingi, "Amecheza namna gani?" - Amecheza *kitoto*. Hali kadhalika, kielezi tumizi *vizuri* kinajibu swali la msingi, "Amefundisha namna gani?" - Amefundisha *vizuri*. Mifano ya vielezi tumizi iliyobaki katika 15(b,d na e) nayo inaweza kufafanuliwa kwa kutumia msingi huu wa kuuliza swali la msingi la namna tendo lilivyofanyika.

### *5.2.4 Vielezi igizi*

Kimsingi, vielezi igizi ni yale maneno yanayotumika kufafanua zaidi jinsi tendo linavyofanyika kwa kuigiza au kufuatisha aina ya mlio unaotokea wakati tendo likifanyika. Mathalani, tunasema mbwa anabweka *bwe*, maji yamemwagika *mwa*. Maneno *bwe* na *mwa* ni vielezi igizi kwa sababu kielezi igizi *bwe* kimetumika kuigiza mlio wa kitendo cha kubweka ambacho kwa kawaida hufanywa na mbwa. Hali kadhalika, kielezi igizi *mwa* pia kimetumika kuigiza mlio wa sauti wa kitendo cha maji kumwagika chini. Vielezi vya aina hii vipo vichache ukilinganisha na aina nyingine za vielezi tulizokwisha zijadili. Chunguza mifano ya vielezi igizi ifuatayo:

20. (a) Babu ameanguka *pu*
    (b) Mbwa wetu hubweka *bwe*
    (c) Mtoto ametumbukia *chubwi* mtoni
    (d) Maji yanachuruzika *chururu*
    (e) Maji yamemwagika *mwa*

Vielezi igizi vyote vilivyotumika katika (20) hapo juu, vinaigiza milio mbalimbali ya sauti zinazoelezea namna ya tendo lilivyofanyika. Tofauti kuu ya *vielezi igizi* na *vielezi halisi* ni kwamba wakati vielezi halisi vina uhusiano wa moja kwa moja na kitenzi na aina nyingine za maneno (vivumishi, vielezi vingine na kwa kiasi fulani nomino na viwakilishi), vielezi igizi havina uhusiano wa moja kwa moja na tendo lenyewe au na aina nyingine za maneno tulizozitaja hapo juu. Kimsingi, dhima ya vielezi igizi ni kuigiza sauti itokanayo na tendo linalotendeka.

## 6.0 Hitimisho

Mjadala wetu mpaka sasa umetuonyesha bayana kwamba maneno tunayoyaita vielezi hayabainishwi kwa sifa za aina moja. Kasoro hii inatufanya tupate vielezi vingi ambavyo hatimaye tunashindwa kuviainisha chini ya msingi mmoja ulio thabiti na imara. Tatizo hili linajitokeza hasa katika kiwango cha kidhahania cha kuelewa dhana ya vielezi. Inatuwia vigumu kwetu kufafanua sawasawa dhana ya vielezi hasa kutokana na ukweli

kwamba maneno tunayoyaita vielezi yameundwa kutoka misingi mbalimbali tofauti. Katika kutatua tatizo hili, makala hii yametambua umuhimu wa tabia ya maneno katika tungo ya kuingiliana na kuathiriana kimaana na kikazi. Badala ya kushikilia kuwa na sifa bainifu za aina moja za vielezi kitu ambacho tunadhani hakiwezekani, makala hii yanapendekeza kuainisha vielezi katika aina kuu mbili.

Aina ya kwanza, tuwe na maneno ambayo ni *vielezi halisi* kwa dhati yake. Maneno haya yawe ndio msingi wa kutupatia sifa bainifu za kuelewa dhana ya vielezi kwa ujumla. Kundi la pili, tuwe na maneno ambayo tuyaite *vielezi tumizi*. Haya yatakuwa ni yale maneno ambayo hayana sifa za msingi za kuitwa *vielezi halisi* lakini yakikaa katika tungo maneno hayo hufanya kazi ya uelezi. Kwa kuzingatia mapendekezo haya, sasa tutakuwa na sifa bainifu za aina mbili. Zile zinazobainisha *vielezi halisi* na zile zinazobainisha *vielezi tumizi*. Kwa kuzingatia sifa bainifu za vielezi tumizi, tunapata aina nne zifuatazo: vielezi tumizi mahali, vielezi tumizi wakati, vielezi tumizi ki-/v- na vielezi tumizi igizi.

## MAREJEO

Ashton, E.O. (1947). *Swahili Grammar*, Including intonation. London: Longman.

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kihore, Y. M. na wenzie (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiwahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Knight, T.W. (1967). *A new Comprehensive English Course*. University of London Press Ltd.

Lyons, J. (1972). *Introduction to Theoretical Linguistics*, Cambridge University Press.

Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili* Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Myachina, E.N. (1981). *The Swahili Language: Language of Asia and Africa Vol.1*. London, Boston na Henly: Routledge and Kegan Paul.

Nkwera, F.M.V. (1978) *Sarufi na Fasihi. Sekondari na Vyuo: Mitaala ya Lugha na Fashihi 4*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.